
# MUHTASARI WA SERA

## Wajibu wa Kimataifa, Uwajibikaji Ndani ya Nchi





Jamii duniani kote zimetumia njia mbalimbali kushirikishana maarifa kuhusu mazingira asilia, namna ya kuyatunza na jinsi ya kutumia rasilimali asilia kwa ufasaha. Hata hivyo, mabadiliko ya haraka ya kijamii, uchumi na mazingira yanachangia jamii na wadau mbalimbali wa mazingira kushindwa kushirikishana maarifa ya uhifadhi waliyonayo na kutengeneza njia za pamoja za utunzaji wa mazingira asilia kwenye maeneo yao. Utafiti tuliofanya kwa kushirikiana na wadau ndani na nje ya maeneo ya kitaaluma unasisitiza kulinda maarifa ya uhifadhi baina ya vizazi yasipotee. Tunasisitiza umuhimu wa ubadilishanaji wa maarifa kwa vizazi, kutengeneza maarifa ya pamoja kwa kuzingatia mambo matatu yaliyoshauriwa katika uundaji wa sera hii kama ifuatavyo.

### Uzalishaji wa maarifa kwa ushirikiano na wadau mbalimbali ili kuleta uelewa wa pamoja.

Uzalishaji wa maarifa ni namna ambayo wadau tofauti wenye uelewa na maarifa mbalimbali kwa pamoja wana badilishana maarifa na uelewa wa jambo. Inaleta usawa na uhusiano wa karibu na inaondoa tofauti kwenye mitazamo na thamani ya jambo miongoni mwa wadau. Inasaidia washiriki kujifunza kutoka kwa kila mmoja kuhusu maarifa na inajumuisha kukubaliana na ubora wa maarifa wanayoshirikishana. Kwa pamoja hii inajumuisha kuimarisha uwezo wa wadau kumiliki njia ya utoaji au ubadilishanaji wa maarifa na maarifa yenyewe. Kwa mfano,uundaji wa maarifa baina ya Vizazi inasaidia vizazi tofauti kupata maarifa na kuthamini maarifa yao ya uhifadhi wa mazingira asilia pamoja na kuimarisha uhusiano wa binadamu na mazingira.

### Kuingiza maarifa yaliyotengenezwa katika ngazi mbali mbali za sera.

Maarifa ya pamoja yanaweza kutambuliwa na kutumika katika ngazi mbali mbali za uundaji wa sera.

Hii itafanikiwa kwa kushirikisha wafanya maamuzi katika ngazi mbalimbali za serekali kwenye ubunifu wa pamoja. Msisitizo zaidi unahitaji kulenga namna ya kuwashirikisha wadau wa ngazi za kijamii na vizazi au makundi rika tofauti katika mchakato mzima kuhakikisha mwitikio, uwajibikaji na kudumu kwa jamii.

Kuingiza maarifa ya pamoja kwenye mipango na kufanya maamuzi itaboresha ushirikiano baina ya wafanya maamuzi, wabunifu wa mawazo na vizazi mbali mbali. Hali hii itasaidia kuboresha ujifunzaji wa pamoja wa muda mrefu na maendeleo mazuri kwenye utaratibu wa kusimamia vyema rasilimali asili.

### Usaidizi wa kitaasisi na kifedha wa ngazi ya chini unahitaji kupatikana

Ushiriki wa Pamoja na ushirikiano unaakisi maarifa na ujuzi washiriki walinao katika shughuli za uhifadhi wa mazingira. Endapo msaada wa kifedha, kitaasisi na nguvu ya Pamoja inawekezwa katika ngazi ya kimataifa, kitaifa na kwa jamii uhifadhi wa mazingira unaweza kufikia hatua nzuri zaidi.

Tunasisitiza umuhimu wa kufadhili mipango ya ushirikiano wa muda mrefu unaoweza kuleta matokeo yenye faida kwa shughili za uhifadhi katika ngazi ya jamii. Taasisi na mifumo ya kifedha inaweza pia kutenga vifungu vya fedha na kuweka mikataba ambayo inahimiza hatua za Pamoja kama vile uundaji wa maarifa, shughuli za ubunifu wa Pamoja kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira na matumizi bora ya rasilimali asilia.

# MUHTASARI WA SERA

## Wajibu wa Kimataifa, Uwajibikaji Ndani ya Nchi







**University of Eastern Finland (UEF)**
Irmeli Mustalahti
Tiina Jääskeläinen
Timo Haapasalo
Ida Herdieckerhoff
Anna Mustonen
Niko Nesterinen
Juni Sinkkonen
Shahid Mallick
Katherine Hall

**Natural Resources Institute Finland (Luke)**
Panu Runko

**Swedish University of Agricultural Sciences (SLU)**
Harry Fischer

**University of Leeds, UK**
Susannah Sallu

**Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Tanzania**
Edda Tandi Lwoga
Ubaldus J. Tumaini
Amaniel Athuman

**Universitas Muhammadiyah Yogyakarta, Indonesia**
Rijal Ramdani

**National Policy Consensus Center, USA**
Kristen Wright
Rebecca McLain

Kundi la utafiti la Responsive Natural Resources Governance (RNRG) lina makao yake kwenye Chuo Kikuu cha Finland Mashariki. Kundi la utafiti la RNRG linapokea fedha za tafiti kutoka kwenye Baraza la Utafiti la Finland na Mfuko wa ufadhili wa Kone. RNRG inaongoza mtandao wa kimataifa wa ushirikikiano na utatuzi wa migogoro ya mazingira (ECCR) ambao kwa sasa unafadhiliwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni ya Finland.
Kwa maelezo zaidiwasiliana na (irmeli.mustalahti(at)uef.fi na edda.lwoga(at)cbe.ac.tz):
https://sites.uef.fi/responsive-natural-resources-governance/